



## MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI TAREHE 8 – 12 APRILI 2024

### MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

**1.Nchini Ivory Coast**, mwishoni mwa mwezi Machi, 2024 takriban tani **215,000** za korosho ghafi zilinunuliwa na kusafirishwa nje ya nchi huku jumla ya tani **130,000** zimenunuliwa na wabanguaji wa ndani ya nchi. Bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima zimeuzwa kati ya Dola za kimarekani **0.45** hadi **0.49** sawa na **Tsh 1,154** hadi **1,257** kwa kilo.

**2.Nchini Ghana** kuna uhaba wa mazao kwa mwaka huu pia kuna kuchelewa kwa mazao msimu wa pili. Hii ni kutokana na joto kali nchini humo linalopelekea kuka kauka kwa maua. Kiasi kidogo cha korosho kinatarajiwa kupatikana mjini Techiman kwa msimu wa pili na ushindani upo juu nchini humo takribani wanunuzi waliosajiliwa kwa ajili ya kununua korosho ni **195**. Bei ya korosho zikiwa kwenye ghala la wasafirishaji imeongezeka kutoka Dola za kimarekani **0.67** hadi **0.74** kwa kilogramu sawa na **Tsh. 1,725** hadi **1,905** kwa kilo kwa korosho ghafi zenye ubora wa ratili **45-46 (45-46 lbs)**.

**3.Nchini Benin** bei za korosho katika ngazi ya mkulima hazijabadilika bado ni Dola za Kimarekani **0.52** hadi **0.53** kwa kilo sawa na **Tsh. 1,339** hadi **1,364**. Aidha, mamlaka zimeendelea kuchukuwa hatua za kutosha kuzuia usafirishaji holela wa korosho kwenda nchi jirani.

**4.Nchini Nigeria** bei ya korosho ghafi katika ngazi ya mkulima zinauzwa kati ya Dola za Kimarekani **0.62** hadi **0.75** sawa na **Tsh 1,596** hadi **1,931** kwa kilo. Hata hivyo taarifa zinaonesha baadhi ya wanunuzi wanalamikia ushuru wa Serikali ni mkubwa nchini humo. Ubora wa korosho hizo bado upo katika kiwango kizuri.

### MWENENDO WA SOKO NCHINI VIETNAM NA INDIA

**1.Nchi ya Vietnam** Bei ya korosho ghafi kutoka Afrika Magharibi zinauzwa kati ya Dola za kimarekani **0.97** hadi **1.06 (CIF-Vietnam)** kwa kilo huku ubora ukiwa ratili **48 (48 lbs)** sawa na **Tsh. 2,488** hadi **2,719** kwa kilo

**2.Nchini India** bei ya korosho ghafi kutoka Afrika Magharibi zinauzwa kati ya Dola za Kimarekani **1.32** hadi **1.36 (CIF-India)** sawa na **Tsh 3,386** hadi **3,488** kwa kilo.

# IMETOLEWA NA BODI YA KOROSHO TANZANIA

S.L.P 533

Mtwara

Simu (Bure) : 0 800 112 159

Nukushi : (023) 2333536

Barua Pepe: [info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)



#Ajenda10/30




Ivory Coast



Ghana



Benin



Nigeria



Vietnam



India